TANGAZO LA SERIKALI NA.1107. la tarehe27/12/2024

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 16(1))*

SHERIA NDOGO YA USHURU WA MAZAO MCHANGANYIKO YA HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA YA MWAKA 2024

Jina

**1.** Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ushuru wa Mazao Mchanganyiko ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa ya Mwaka 2024.

Matumizi

**2.** Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa.

Tafsiri

**3.** Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"afisa mwidhiniwa" maana yake ni afisa aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"gulio" maana yake ni eneo au sehemu yoyote ya wazi au iliyojengwa ambayo imetengwa na Halmashauri kwa ajili ya shughuli za kuuza na kununua mazao na bidhaa nyingine, na itajumuisha chama cha ushirika cha msingi kilichoteuliwa kuuza mazao mchanganyiko;

"Halmashauri" maana yake Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa;

"mazao mchanganyiko" maana yake ni mazao ya chakula, mazao ya biashara na mazao ya misitu na maliasili ambayo huzalishwa na kupatikana katika eneo la Halmashauri, isipokuwa zao la korosho;

Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa au afisa aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mnunuzi" maana yake ni mtu binafsi, kikundi cha watu au taasisi yoyote inayojishughulisha na ununuzi wa mazao mchanganyiko katika eneo la Halmashauri kwa nia ya kufanya biashara;

"msafirishaji" maana yake ni mtu binafsi, kampuni au taasisi inayosafirisha mazao mchanganyiko;

"muuzaji" maana yake ni mtu binafsi, kikundi cha watu, kampuni au taasisi inayojishughulisha na uuzaji wa mazao mchanganyiko katika eneo la Halmashauri;

"ushuru" maana yake ni malipo yanayotozwa na kulipwa kwa Halmashauri kama kodi ya bidhaa au huduma inayotolewa;

"wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi cha watu, kampuni au taasisi iliyoingia mkataba kutekeleza Sheria Ndogo hii kwa niaba ya Halmashauri.

Utozaji wa ushuru

**4**.-(1) Halmashauri itatoza ushuru wa mazao mchanganyiko kwa kiwango cha asilimia tatu (3%) ya bei ya kununulia mazao kwa ajili ya mazao yote yanayosafirishwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hii utalipwa kwa Halmashauri na utakusanywa na Halmashauri au wakala kadri Halmashauri itakavyoelekeza.

(3) Mtu yeyote hataruhusiwa-

(a) kununua au kusafirisha mazao bila kulipia ushuru; au

(b) kuuza au kununua mazao mchanganyiko katika eneo ambalo si gulio.

Wajibu wa kulipa ushuru

**5.** Mtu anayepaswa kulipa ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii atalipa kwa kuzingatia kiwango kilichoainishwa katika kanuni ya 4 na hataruhusiwa kununua mazao katika eneo la Halmashauri bila kuwa na leseni ya biashara iliyoidhinishwa na Halmashauri.

(2) Mtu yeyote anayekusudia kusafirisha mazao kutoka katika eneo la Halmashauri atapaswa kuwa na kibali maalum cha kusafirishia mazao kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

Malipo ya ushuru

**6**.-(1) Malipo ya ushuru yatafanyika kabla au wakati wa kupokea huduma inayotozwa ushuru chini ya Sheria Ndogo hii.

(2) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1), ushuru unaweza kulipwa muda wowote katika siku husika, mwezi husika au kwa namna nyingine itakayokubalika baina ya Halmashauri na mlipa ushuru.

Stakabadhi za malipo za kieletroniki

**7.-(**1) Halmashauri itatoa stakabadhi ya kielektroniki kwa ushuru utakaotozwa na kulipwa kama ushahidi wa malipo yaliyofanyika kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(2) Kila mlipa ushuru wa mazao mchanganyiko atakuwa na wajibu wa kudai na kuhakiki stakabadhi ya malipo kulingana na kiasi cha fedha alicholipa.

Ukusanyaji wa madeni

**8**.-(1) Endapo mlipa ushuru atashindwa kulipa ushuru wa mazao mchanganyiko ndani ya muda aliopewa na hivyo kusababisha deni, Halmashauri baada ya kupata amri ya mahakama inaweza kukusanya deni hilo kwa kukamata mali zenye thamani sawa na deni la ushuru pamoja na gharama za kukamata za mtu binafsi, kikundi, kampuni au shirika lililoshindwa kulipa deni husika

(2) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuuza mali za mdaiwa kwa njia ya mnada baada ya siku thelathini kupita tangu kukamatwa kwa mali za mdaiwa.

(3) Kwa mali zinazoweza kuharibika kwa haraka, Halmashauri baada ya kupata kibali cha mahakama itakuwa na uwezo wa kuuza mali hizo kabla hazijaharibika.

(4) Bila kuathiri masharti ya kanuni hii, kabla ya kuuza mali yoyote iliyokamatwa, Halmashauri itatoa taarifa ya siku zisizozidi saba kwa mdaiwa na umma kuhusu kusudio la kuuza mali hizo.

(5) Halmashauri haitawajibika kwa hasara itakayotokea wakati wa kukusanya madeni au kwa mali itakayokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri, isipokuwa kama hasara hiyo itakuwa imesababishwa na uzembe wa watumishi wa Halmashauri au wakala.

Uteuzi wa Wakala

**9**.-(1) Halmashauri inaweza kuteua wakala kwa ajili ya kutekeleza majukumu chini ya Sheria Ndogo hii.

(2) Wakala atakayeteuliwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) atakuwa na wajibu wa:

(a) kukusanya na kupokea ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoidhinishwa katika Sheria Ndogo hii; na

(b) kukusanya ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Mamlaka ya kuingia katika eneo la biashara

**10.** Mkurugenzi au afisa mwidhiniwa atakuwa na mamlaka ya kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kwa muda wowote kwa nia ya kukusanya ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Bidhaa iliyokamatwa pasipo kulipiwa ushuru

**11.-**(1) Halmashauri itatoza kwa kila siku kiasi cha asilimia tano ya thamani ya bidhaa iliyokamatwa ikisafirishwa pasipo kulipiwa ushuru.

(2) Mmiliki wa bidhaa iliyokamatwa asipolipa ushuru husika ndani ya siku saba kuanzia siku ambayo bidhaa imekamatwa, Halmashauri itauza bidhaa husika kwa njia ya mnada kwa ajili ya kufidia gharama za kukamata, kuhifadhi bidhaa na ushuru unaodaiwa.

(3) Kwa madhumuni ya kanuni ndogo ya (2), masharti yaliyowekwa kwenye kanuni ya 8 yatatumika.

Muda wa ununuzi

**12**.-(1) Muda wa kununua na kuuza mazao utaanza saa kumi na mbili alfajiri na kuisha saa kumi na mbili jioni.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Halmashauri au Wakala, kwa kibali maalum kutoka kwa

Mkurugenzi, anaweza kuuza au kununua mazao baada ya muda uliotajwa.

Makosa

**13**.-(1) Mtu atatenda kosa endapo-

(a) atashindwa kulipa ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ushuru;

(c) atamzuia Mkurugenzi, afisa mwidhiniwa au wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(d) atatoa taarifa za uongo kwa Mkurugenzi, afisa mwidhiniwa au wakala kuhusu huduma zinazohitaji kulipiwa ushuru;

(e) atashindwa kuweka kumbukumbu au maelezo yoyote yatakayohitajika na Halmashauri;

(f) atashindwa, atadharau, atakaidi au kukataa kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kuhusiana na ulipaji wa ushuru chini ya Sheria Ndogo hii;

(g) atatengeneza, atatayarisha, ataidhinisha kutengeneza au atatunza nyaraka za uongo kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa ushuru ndani ya Halmashauri; au

(h) atatumia chombo chochote kusafirishia bidhaa ambayo haijalipiwa ushuru.

(2) Wakala aliyeteuliwa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii atatenda kosa endapo-

(a) atatumia nyaraka za kugushi kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa ushuru ndani ya Halmashauri;

(b) atashindwa kutoa taarifa au atatoa taarifa za uongo Halmashauri kuhusu bidhaa au huduma zinazotakiwa kulipiwa ushuru;

(c) hatawasilisha au atawasilisha kwa kuchelewa makusanyo ya ushuru Halmashauri kulingana na muda aliopewa kwa mujibu wa mkataba; au

(d) atashindwa kutunza kumbukumbu sahihi za malipo ya ushuru.

Adhabu

**14**.-(1) Mtu atakayepatikana na hatia kwa kutenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini na isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichopungua miezi sita jela na kisichozidi miezi kumi na mbili jela au vyote kwa pamoja.

(2) Endapo mtu aliyepatikana na hatia ni wakala, pamoja na adhabu iliyoainishwa katika kanuni ndogo ya (1) atalipa Halmashauri kiasi cha pesa alizopaswa kulipa au zilizopaswa kulipwa na mlipa ushuru.

Kufifilisha kosa

**15.** Mkurugenzi anaweza kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii kiasi kisichozidi shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kujaza fomu maalumu kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4(2))*

MAZAO MCHANGANYIKO YATAKAYOLIPIWA USHURU

| Na. | MAZAO | KIASI CHA USHURU |
|---|---|---|
| 1. | Mahindi | 3% ya bei ya kununulia mazao |
| 2. | Mpunga | |
| 3. | Ufuta | |
| 4. | Mbaazi | |
| 5. | Kunde | |
| 6. | Choroko | |
| 7. | Maharage | |
| 8. | Machungwa | |
| 9. | Nanasi | |
| 10. | Ndizi | |
| 11. | Machenza | |
| 12. | Tikiti | |
| 13. | Nyanya | |
| 14. | Vitunguu | |
| 15. | Maembe | |
| 16. | Nazi | |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 5(2))*

KIBALI CHA KUSAFIRISHA MAZAO

Namba ya kibali…………………….. Tarehe ……………………...

Msimu…………………………. Zao ………………………
Jina la mnunuzi……………………………………………………………………..
Idadi ya Tani/Kilo za awali…………………………………………………………
Kiasi kilichonunuliwa………………………………………………
Jumla ya Tani/Kilo……………………………………………………………….
Kiasi kinachosafirishwa……………………………………………………………
Kiasi kilichobaki…………………………………………………………………..
Namba ya stakabadhi ya ushuru……………………………………………………..
PDN ya chama cha msingi/Stakabadhi………………………………………………
Tarehe ya kusafirisha………………………………………………………………..
Jina la Dereva………………Na. ya Gari………………
Jina la Afisa aliyeidhinisha mzigo……………………….Saini………………………
Mhuri na saini ya Mkurugenzi/Mweka hazina

---

JEDWALI LA TATU

---

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 15)*

FOMU YA KUKIRI KOSA

Mimi ……………………………………………………..………… NAKIRI KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya …………………………….ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Wilaya ya Kilwa, kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi ……. mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kanuni ya …… ya Sheria Ndogo ya Ushuru wa Mazao Mchanganyiko ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa ya Mwaka 2024.

NAKUBALI kulipa ushuru ninaodaiwa kwa kiasi cha shilingi ..................... pamoja na faini ya kufifilisha kosa kwa kiasi cha shilingi ...................

NATHIBITISHA KWAMBA, maelezo niliyotoa hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa MIMI MWENYEWE na kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.

Leo hii tarehe………….ya mwezi…………..… mwaka 20…………….
Jina……………………………….....
Saini……….......………………......

MBELE YA MKURUGENZI

Jina:………………….....................................
Saini:…………………..….............................
Tarehe:..............................................................

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa imegongwa kwenye Sheria ndgo hizo kufuatia azimio lililopitishwa katika Mkutano mkuu wa baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya kilwauliofanyika tartehe 9/11/2023 na kushuhudiwa Lakiri hiyo ikigongwa mbele ya:-

HANAN M. BAFAGHI,
*Mkurugenzi Mtendaji,*
*Halmashauri ya wilaya,*
*Kilwa*

MHE. ISSA B. MATEKA,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya wilaya,*
*Kilwa*

L.S

**NAKUBALI**,

Dodoma,
29 Oktoba, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI*